# HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA.

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19 KWA KUTUMIA MAPATO YA NDANI**

**KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU**



**IMEANDALIWA NA:**

MKURUGENZI WA JIJI,

HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA,

S.L.P 178;

TANGA

March 2019.

**CONTACT NO.**

1. +255 715639797 CITY ECONOMICS
2. +255 759254002 CITY PUBLIC RELATION OFFICE

YALIYOMO

UTANGULIZI.......................................................................................................3

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ...............................................................4

IDARA YA KILIMO. .........................................................................................................4

IDARA YA UTAWALA.......................................................................................................4

IDARA YA AFYA. ............................................................................................................6

IDARA YA MAPATO. .......................................................................................................8

IDARA YA MAENDELEO YA JAMII. ....................................................................................8

IDARA YA ARDHI. ..........................................................................................................9


2.0 CHANGAMOTO. ........................................................................................................12

2.1 Utatuzi wa Changamoto hizo; .....................................................................................12

TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA NA FEDHA ZA MAKUSANYO YA NDANI. Januari - Machi 2018 ................................................................................1

## 1.0 UTANGULIZI.


Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Bajeti ya Halmashauri ya Jiji la Tanga ilikasimia kutengakiasi cha **Tsh. 15,192,895,032/=**kutoka vyanzo vya ndani vya mapato ya Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi ya maendeleo pamoja na matumizi mengineyo ya ofisi.Baada ya kutoa mapato fungwa ya jumla ya **Tshs 2,716,965,507** kiasi kinachobaki cha **Tshs 12,475,929,525/=** Asilimia 40 ya kiasi hicho jumla ya **Tshs 4,990,371,910/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Halmashauri na asilimia 60 ni kwa jaili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na **Tshs 7,485,557,715/=**Picha ifuatayo inaonyesha mgawanyo wa fedha hizo za makusanyo ya ndani pamoja na mgawanyo wake.



## 2.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO


### 2.1 IDARA YA KILIMO.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, Idara ya Kilimo ilitenga kiasi cha **Tsh 220, 000,000/=** kwa ajili ya matumizi ya miradi ya idara ya Kilimo. Hadi kufikia tarehe 30 Machi,Idara imeweza kutumia jumla ya **Tshs.52,548,600/=** kwa ajili ya kuwezesha ushiriki wa mafunzo ya kilimo na maonyesho ya nanenane pamoja na kilimo cha umwagiliaji. Mashine ya umwagiliaji imenunuliwa na vimefungwa kwa kipindi husika kwa gharama hizo.




### 2.2 IDARA YA UTAWALA.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2018/2019,** Idara ya Utawala ilitenga kiasi cha **Tsh 2,216,727,516/=** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi wa miradi ya maendeleo. Jumla ya **Tshs 436,915,735/=** imetekeleza ujenzi wa miundombinu mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa jengo la utawala la ghorofa 3 na kurekebisha majengo ya TADECO.






*Picha1.1: Jengo la utawala la jiji la Tanga.*

### 2.3 IDARA YA AFYA.


Katika kipindi cha mwaka wa fedha **2018/2019,** Idara ya Afya ilitenga kiasi cha **Tsh 556,400,000/=** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi katika idara ya afya zikiwemo ujenzi wa kituo cha afya cha Mwakidila,Kuchangia ujenzi wa hospital ya Wilaya ambayo utekelezaji wake unaendelea,Kuchangia kwenye miradi ya UKIMWI, uendeshaji wa duka la dawa na ukarabati wa ofisi ya CHF ya Jiji.Jumla ya **Tshs 8,139,050/=** imetumika kutekeleza miradi hiyo.



*Ujenzi wa kituo cha Afya Mwakidila kikiwa usawa wa mtambaa panya kwa fedha za mapato ya ndani.*




*Ujenzi wa hospital ya Wilaya Tanga. Mojawapo ya majengo ya Hospital ya Wilaya ambao fedha za mapato ya nadni zinatumika kwa ajili ya ufuatiliaji wa mradi huo.*




## 2.4 IDARA YA MAPATO.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, Idara ya Mapato ilitenga kiasi cha **Tsh 623,103,192/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya idara ya fedha Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni Ununuzi wa magari mawili kwa ajili ya kusaidia ukusanyaji wa mapato,kujenga masoko ya jiji na ununuzi wa POS mashine .Miradi iliyotekelezwa ni ununuzi wa POS mashine 40 pamoja na kujenga choo katika soko la Makorora. Utekelezaji huo umegharimu jumla ya **Tshs 48,900,000/=**





## 2.5 IDARA YA MAENDELEO YA JAMII.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, Idara ya Maendeleo ya Jamii ilitenga kiasi cha **Tsh.960,206, 961/=** kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na walemavu kwa kufuata kanuni ya asilimia 4,4,2.Hadi kufikia Juni 2019, jumla ya **Tshs274,500,000/=** zimetolewa kwa vikundi vya wanawake na vijana. Wanawake walipata jumla ya **Tshs 254,500,000/=** na vijana **Tshs 20,000,000/=**





**2.6 IDARA YA ARDHI.**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, Idara ya Ardhi ilitenga kiasi cha **Tsh 1,400,000,000/=** kwa ajili ya kuwezesha mchango wa utoaji wa ardhi kwa viwanja 10 na mahitaji mengine ya maendeleo ya ardhi katika eneo la Amboni katika Mji wa Tanga ifikapo Juni 2019. Jumla ya **Tshs 426,676,694.80** zimetumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za idara ya Ardhi ikiwemo kupima viwanja katika maeneo ya Amboni na Kange Kasera.



## 2.7 IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI.

Idara ya Uchumi ni idara ambayo inatekeleza na kusimamia na kufuatilia miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa katika Halmashauri. Ili kuweza kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi, Idara ilitengewa jumla ya **Tshs 1,075,661,208/=** kwa ajili ya utekelezaji wamiradi, usimamizi na ufuatiliaji. Kati ya hizo jumla ya **Tshs 504,231,648/=** zimetumika kutekeleza miradi hiyo. Miradi iliyotekelezwa ni uwezeshaji wa kituo cha Tanga Televishen,Mchango kwenye miradi ya TASAF,TACINE, UKETA,TSCP, kuwezesha shughuli za uwezeshaji, Kuandaa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020,urekebishaji wa vyoo vya umma, Kujenga kituo cha daladala Pongwe pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi yote inayoendelea kutekelezwa.






Kibanda cha mashine ya kufyatulia matofali

## 2.8 ELIMU

Idara hii ni idara ambayo imebeba idara mbili ambazo ni idara ya Elimu Msingi na Elimu Sekondari. Idara hizi kwa pamoja zimetengewa jumla ya **Tshs 1,044,467,955/=** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya vyumba vya madarasa, vyoo na maabara.Jumla ya **Tshs 132,416,825/=** zimetumika kutekeleza miradi hiyo kwa kipindi cha Januari hadi Machi



## 3.0 **CHANGAMOTO.**

- Muitikio mdogo wa wananchi kuchangia miradi ya maendeleo kama vile upande wa elimu juu ya dhana ya elimu bure.
- Baadhi ya wafanya biashara kukwepa kulipa kodi kwenye vyanzo vya mapato na hiyo kupelekea kutofikiwa kwa asilimia 100ya makusanyo.
- Pia vyanzo Vingine vya mapato kufutwa katikati ya mwaka wa fedha na hivyo kuathiri kiwango cha ukusanyaji mapato

## 3.1 **Utatuzi wa Changamoto hizo;**

1. Kuongeza ununuzi wa mashine za kukusanyia mapato ili kuweza kufikia vyanzo vyote vya mapato ya ndani na kukusanya ipasavyo.
2. Kubuni vyanzo vipo vya mapato kwa kuanzisha miradi mikubwa ya kimkakati ili kuweza kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato

| TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA NA FEDHA ZA MAKUSANYO YA NDANI. Januari - Machi 2018 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| **Sekta** | **Jina la mradi.** | **Fedha iliyoidhinishwa** | **Fedha iliyotolewa** | | | **Hali ya utekelezaji** | **Baki** | **Maelezo.** |
| | | | **Halmashauri** | **Wananchi** | **Jumla** | | | |
| ELIMU | Kuchangia ujenzi/ kukarabati miundombinu ya shule za walemavu Jijini Tanga | 100,000,000 | 5,715,636.80 | | 5,715,636.80 | Utekelezaji umefanyika | 0 | Utekelezaji umefanyika |
| | Kujenga/ kumalizia maabara kwa shule za Sekondari | 400,000,000 | 30,000,000 | 0 | 30,000,000 | Utekelezaji umefanyika | 0 | Imetekelezwa |
| | Kujenga madarasa kwa shule za Msingi | 344,467,955 | 66,701,189 | 0 | 66,701,189 | Ujenzi wa madarasa 6 umefanyika | 0 | Imetekelezwa |
| Kilimo | kuwezesha maandalizi na ushirikiano wa maonyesho ya kilimo ya Nane Nane Juni 2019 | 220,000,000.00 | 52,548,600 | 0 | 52,548,600 | ununuzi wa mashine ya umeme ulifanyika katika maonyesho ya Nanenane | 0 | Utekelezwaji umekamilika. |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Morogoro | | |
| UTAWALA | Kujenga na kurekebisha majengo ya Halmashauri na ukuta wa makao makuu mnamo Juni 2019 | 400,000,000.00 | 85,570,360 | 0 | 85,570,360 | Fedha ilitolewa ili kurekebisha majengo ya TADECO na ujenzi wa mashine ya Block | 0 | Ujenzi na ukarabati miundombinu wa umefanyika |
| | Kuweka / kuimarisha miundombinu ya taa za barabarani | 100,000,000 | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 | Imetekelezwa | | Umefanyika |
| | Kuwezesha shuhuli za ulinzi na usalama ngazi ya Wilaya na ngazi ya Msingi | 239,997,600 | 65,635,989 | 0 | 65,635,989 | Uwezeshaji umefanyika | 0 | Imetekelezwa |
| | Kuwezesha mbio za Mwenge wa Uhuru Wilayani | 70,000,000 | 70,000,000 | 7,200,000 | 77,200,000 | Utekelezaji umefanyika | | Imetekelezwa |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| AFYA | Kujenga majengo 4 ya OPD katika vituo vya Afya vya Mwanzange, Kisimatui, Geza na Kiomoni mwezi Juni 2019 | 300,000,000.00 | 8,139,050 | 0 | 8,139,050 | Kukamilika kwa zahanati ya Nguvumali | 0 | Ujenzi wa zahanati ya Nguvumali umekamilika. |
| FEDHA/ MAPATO | Ununuzi wa vifaa vya ki-elekroniki vya ukusanyaji mapato (POS) | 80,000,000.00 | 33,900,000 | 0 | 33,900,000 | Kununua POS za ukusanyaji mapato zipatazo 40 | 0 | POS mashine zipatazo 40 zimenunuliwa na zinatumika |
| FEDHA/ MAPATO | Kujenga masoko ya Jiji | 400,000,000 | 15,000,000 | 0 | 15,000,000 | Utekelezaji umefanyika katika soko la Makorora kwa kujenga choo | 0 | Imetekelezwa |
| Maendeleo ya Jamii | Kutoa mkopo kwa makundi 210 ya wanawake ifikapo Juni 2019 | 381,031,006.72 | 254,500,000 | 0 | 254,500,000 | Mikopo ilitolewa kwa makundi 75 ya wanawake | 0 | Mikopo ilitolewa kwa makundi 75 ya wanawake |
| Maendeleo ya Jamii | kutoa mkopo kwa makundi 210 ya vijana ifikapo Juni 2019 | 381,031,006.72 | 20,000,000 | 0 | 20,000,000 | Makundi 8 ya vijana walipata mkopo | 0 | Makundi 8 ya vijana walipata mkopo |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ARDHI | kuwezesha mchango wa utoaji wa ardhi kwa viwanja 10 na mahitaji mengine ya maendeleo ya ardhi katika eneo la Amboni katika mji wa Tanga ifikapo Juni 2019 | 1,400,000,000.00 | 426,676,695 | 0 | 426,676,695 | utoaji wa ardhi kwa ajili ya viwanja 10 na mahitaji mengine ya maendeleo ya ardhi katika eneo la Amboni kufanyika | 0 | utoaji wa ardhi kwa ajili ya viwanja 10 na mahitaji mengine ya maendeleo ya ardhi katika eneo la Amboni umefanyika |
| Uchumi | Kuwezesha kituo cha TaTV | 180,000,000.00 | 80,490,600 | 0 | 0 | Ujenzi wa fensi umefanyika | 0 | Utekelezaji umeafanyika |
| | Kuchangia kwenye mradi wa TASAF | 10,000,000 | 4,806,000 | 0 | 4,806,000 | Uwezeshaji wa shughuli za TASAF umefanyika | | Imetekelezwa |
| | Kuwezesha shughuli za Uwekezaji | 89,000,000 | 64,824,700 | 0 | 64,824,700 | Utekelezaji umefanyika | | Imetekelezwa |
| | Kuandaa Mpango na Bajeti ya Halmashauri 2019/2020 | 139,070,000.00 | 68,704,000.00 | 0 | 68,704,000.00 | Utekelezaji umefanyika | | Bajeti imeandaliwa |
| **UCHUMI** | Kusimamia na kufuatilia miradi ya maendeleo | 144,060,484.00 | 65,875,180.00 | 0 | 65,875,180.00 | Usimamizi na ufuatiliaji umefanyika | | Imetekelezwa |
| | Kuandaa taarifa | 43,500,000 | 36,743,600 | 0 | **36,743,600** | Utekelezaji | | Utekelezaji |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | za LAAC na kujenga uwezo wa mifumo | | | | | umefanyika | | umefanyika |
| | kuwezesha utekelezaji wa mradi wa TSCP | 20,200,000.00 | 13,662,120 | 0 | 13,662,120 | Uwezeshaji umefanyika | | Imetekelezwa |
| | Kujenga na kurekebisha vyoo vya umma mnamo Juni 2019 | 200,000,000 | 137,267,016 | 0 | 137,267,016 | Utekelezaji umefanyika katika shule ya Msingi Bombo | | Imetekelezwa |
| | Kuendeleza miundombinu ya soko la wajasiriamali Mwahako na stendi ya daladala Pongwe | 200,000,000 | 10,711,332 | 0 | 10,711,332 | Kituo cha daladala Pongwe kimejengwa | **0** | Imetekelezwa |
| | Kuchangia kwenye mradi wa UKETA | 8,501,250 | 7,860,000 | | 7,860,000 | Uwezeshaji watumishi umefanyika | **0** | Uwezeshaji watumishi umefanyika |
| | Kuchangia kwenye mradi wa TACINE | 21,329,474 | 13,287,100 | | 13,287,100 | Uchangiaji umefanyika | | Imetekelezwa |
| **JUMLA** | | **7,423,632,916.00** | **1,700,203,106** | **0** | **1,700,203,106** | | **0** | |